

Learning by Ear 2010 – Urban Exodus – “Against the Current”**Episode 06: “Caught between pressure and constraints”****Author: Alfred Dogbé****Editor: Yann Durand****Translator: Anne Thomas**

WAHUSIKA:

Onyesho la 1:

- BEN** (MHANDISI WA KILIMO, UMRI MIAKA 29)
- KABO** (MKULIMA, MJOMBAKE BEN, UMRI MIAKA 57)
- BAKI** (UMRI MIAKA 26, MWANAELIMUJAMII, RAFIKI YAO ZEINA NA BEN)
- ZEINA** (UMRI MIAKA 24, MCHUMI, RAFIKI YAO BAKI NA BEN)
- NANA** (UMRI WA MIAKA 22, KIONGOZI WA CHAMA CHA VIJANA)

Onyesho la 2:

- BEN** (MHANDISI WA KILIMO, UMRI WA MIAKA 29)
- TINGO** (UMRI WA MIAKA 32, MKULIMA WA KISASA)

Onyesho la 3:

- BEN** (MHANDISI WA KILIMO, UMRI MIAKA 29)
- NANA** (UMRI MIAKA 22, KIONGOZI WA CHAMA CHA VIJANA)

Intro :

Karibu kwenye mfululizo huu mpya wa *Learning by Ear*. Kipindi cha leo ni cha sita cha mfululizo wa michezo ya redio kuhusu uhamiaji mijini uitwao “Kukabiliana na Wimbi la Mabadiliko”.

Tunafuatilia masaibu ya Ben, Baki na Zeina – vijana watatu wasio na ajira walio na shahada za chuo kikuu ambao wameamua kuanzisha chama cha ushirika cha ukulima kijijini ili kuondokana na dhiki ya ukosefu wa ajira mjini.

Wahusika wetu hatimaye wametayarisha muundo wa chama katika mkutano mkuu ambao ulihudhuriwa na baadhi ya wanakijiji. Hata hivyo, ni jambo linalohitaji mchakato mrefu na kwenye kipindi hiki cha sita tutashuhudia vikwazo vipya ambavyo Ben na kundi lake watakabiliana navyo.

Scene 1: At Ben’s. Morning.**KABO, BEN, ZEINA, BAKI AND NANA**

- 1. ATMO: MORNING AT BEN’S. HENS – LITTLE TRAFFIC – INSTRUMENTAL MUSIC FROM THE RADIO AT LOW VOLUME**
- 2. KABO** Ninawapa hongera, wanangu! Kikao cha baraza kuu kimefanikiwa sana. Jamaa wote wa kijijini walikuwepo. Mjadala ulikuwa mkali. Mjadala maalumu. Sikumbuki mara ya mwisho nilipowaona wanakijiji wakihoji kuhusu maisha yao, na mustakabali wao. Sikuamini kwamba baadhi yao ni wale wale wanakijiji niwajuao.

3. **BEN** Kweli usemayo! Tunakushuru wewe na Nana kwa kufaulu kote huko.
4. **NANA** Lakini nadhani wanawake wengi zaidi wangehudhuria.
5. **BAKI** Walikuwa wamealikwa.
6. **ZEINA** Siku zijazo itatubidi kutafuta mbinu nyingine za kuwahamasisha na pia kuwatengea nafasi watoe maoni yao.
7. **NANA** Hapana, tusiwatengee wanawake maeneo yao.
8. **BAKI** Kweli hayo!
9. **ZEINA** Wajua kina mama wengi hawawezi kuja kwa kuwa waume zao watawataka wabaki nyumbani wakati wao, wanaume, wanapokuwa mkutanoni.
10. **KABO** Hiyo ni kweli! Lakini inasemekana kwamba waliohudhuria hawakuja tu kushangalia. Walishughulika kwa dhati.
11. **NANA** Na walitoa maoni yao kuhusu maswala kadha muhimu!
12. **ZEINA** Ndiyo hivyo, inatubidi tuwape kina mama nafasi zaidi ya kujihusisha na mradi.
13. **BEN** Naona bora tuanzishe kundi la kuwahamasisha kina mama.
14. **NANA** Nitajitolea kutekeleza jukumu hilo. Je, Mjomba Kabo uko tayari kushirikiana nami?
15. **KABO** Bila shaka.

16. **NANA** Tutawategemea kina mama wachache ambao tayari wanajihusisha.
17. **BAKI** Muhimu katika mkakati wetu ni kuwavutia watu, kwa vitendo vyetu vizuri ili watathmini mafanikio ya chama chetu.
18. **ZEINA** Miradi mingi huanza kwa kasi, ikaja kukwama baadaye. Mwishowe hakuna cha hamasa wala matumaini.
19. **BAKI** Hatuna budi ila kuhakikisha kwamba tumetenda jambo la faida linaloonekana ili wakazi wazidi kuwa na moyo wa kujihusisha.
20. **NANA** Tunapaswa kuwa watu wa vitendo. Ni lazima tuzindue mara moja mradi utakaowavutia watu kwa msingi wa maadili na malengo ambayo tayari tumekwisha kuwaeleza.
21. **ZEINA** Kuna jambo jingine la dharura! Hatuna hata senti moja kwenye hazina yetu. Tusipolitatia tatizo hilo, shughuli za chama chetu zitatatizika
22. **BEN** Nani ana pendekezo?
23. **ZEINA** Itatubidi kuwa na ada ya uanachama. Sijui kwa nini hatukulitaja hili kwenye mkutano mkuu.
24. **BAKI** (**aggressively**) Mbona hukutaja?
25. **BEN** Acheni kubishana. Hatukugusia mambo yote tuliyokuwa tumeorodhesha kwa kuwa kila mtu alitaka kuchangia.

- 26. ZEINA** Hata hivyo... tulipaswa kulizungumzia suala hili muhimu...
- 27. NANA** Ni suala muhimu. Tusipojihadhari huenda watu wakachukulia kwamba chama hiki kimeanzishwa kuwapa wanakijiji maskini msaada wa kifedha kama yanavyofanya baadhi ya mashirika yasiyo ya kiserikali.
- 28. BAKI** Huo ndio mwanzo wa mizozo na kusambaratika chama chetu.
- 29. KABO** Sote tumo katika kipindi cha mpito. Jamaa wengi wamefungukiwa na chakula. Tukiwaomba walipe ada ya uanachama, watatuona wendawazimu!
- 30. NANA** Kusema kweli!
- 31. BAKI** Lakini wanachama wote ni lazima watoe mchango mahsusi. Inatubidi kuwa na msimamo!
- 32. KABO** Lakini hatuwezi kuwaambia mambo ya pesa.
- 33. BEN** Watoe mchango gani basi?
- 34. NANA** Hilo litategemea shughuli tunayonua kufanya. Na hilo linanikumbusha, Ben umefikia wapi?
- 35. BEN** Niko karibu kukamirisha mradi kuhusu mbinu za kukabiliana na uharibifu wa udongo. Hicho ndicho kikwazo kikubwa kwenye ukulima na hili tunaweza kulishughulikia kwa kasi na pia kuwashawishi wanakijiji watuunge mkono.
- 36. ZEINA** Tuelezee zaidi...

- 37. BEN** Maeneo mengi yanayoshughulikia kilimo yamekuwa yakipungukiwa na mazao kila mwaka kwa sababu ya kutumiwa zaidi, ukosefu wa virutubishi kwenye udongo na pia maeneo ya malisho ya mifugo. Ninaandaa utaratibu na mbinu endelevu za kilimo ili kuanzisha mfumo utakaojumuisha masuala ya kibaiolojia, kijamii na pia kibinadamu.
- 38. BAKI** Sijaelewa lolote. Nifafanulie jinsi wanakijiji watakavyofaidika moja kwa moja.
- 39. BEN** Nitawahimiza warejeele mbinu fulani za kienyeji, wakuze aina fulani ya mimea na pia wapande mimea mipya kuimarisha rutuba ya udongo wa ardhi ili mazao yao yaongezeke. Nitawafanulia wazo zima pindi nitakapomaliza kulishghulikia.
- 40. KABO** Sasa hivi, mimi na Baki tutakwenda kwa mkuu wa kijiji tukajulie suala la shamba.
- 41. BAKI** Twende!
- 42. ZEINA** Tutaonana baadaye!
- 43. BEN** Kila la heri!
- 44. SFX: STEPS GOING AWAY**

----- MUSIC -----

Scene 2: In town. A bar.**BEN AND TINGO.****45. SFX: A BAR IN TOWN. CONVERSATION, MUSIC IN THE BACKGROUND. TRAFFIC, CAR HORNS**

46. TINGO Hujambo. Habari gani Bwana Ben?

47. BEN Naam, mimi Ben. Wewe nani?

48. TINGO Hunijui mimi? Ninaitwa Tingo. Mimi ndiye mwenye shamba maarufu katika eneo hili linalotumia mbinu za kisasa...

49. BEN Alaa!

50. TINGO Vyema ukinitembelea. Shamba lenyewe zuri.

51. BEN Utaniwia radhi, hapa kuna mtu ninayemsubiri.

52. TINGO Unanisubiri mimi. Nimehiari kuja hapa. Hali ya maisha kijijni si mchezo. Nashukuru kwamba umefika ingawa dhiki za hapa si haba. Nipe dakika chache nikweleze nililokuitia..

53. BEN Wasemaje?

54. TINGO Nimekuja kukupongeza kwa kuanzisha chama cha ushirika. Ni suala linalohitaji ukakamavu wa hali ya juu na pia lina gharama zake – maanake linahitaji muda na kujitolea. Nami nina jambo ningependa kukupendekezea ili mpate kuzindua chama chenu.

55. BEN Kweli. Jambo gani hilo?

- 56. TINGO** Aha! Naona uko tayari, siyo? Si mchezo. Ni biashara kubwa. Mimi ni mkulima wa njugu. Mimi huuza zao langu Ulaya ambako nina mteja anayenunua zao langu kwa wingi. Mimi hukuza njugu kisha humuuzia mavuno yote nipatayo. Ni biashara nzuri ambayo ina faida kubwa hasa ukizingatiya vizingiti tunavyokumbana navyo-mvua isiyotabirika, wadudu na masoko. Unanipata?
- 57. BEN** Hayo unayoniambia yananihusu vipi?
- 58. TINGO** Ni hivi. Ninakupa kandarasi hiyo hiyo. Mkataba wa kuwasilisha tani elfu 30 za njugu kwa bei nzuri isiyobadilika. Si hayo tu. Ukikubali nitakulipa nusu ya kiasi cha hiyo bei.
- 59. BEN** Tunataka kulima mimea ya chakula.
- 60. TINGO** Hundi hii hapa! Kwa kiasi hiki chama chenu kitaanza kufanya kazi.
- 61. BEN** (**in a dry tone**). Ebu sikia nikwambie! Lengo moja kuu la chama chetu cha ushirika ni kupunguza njaa hapa kijijini kwetu na viunga vyake.
- 62. TINGO** Ukiwagawia fedha hizi wanachama wa chama chenu, njaa itatoweka kabisa.
- 63. BEN** Unajua vizuri kwamba unayosema hayana msingi!
- 64. TINGO** Unazihitaji fedha? Ndiyo au la?
- 65. BEN** Ndiyo, chama kinahitaji fedha. Tena fedha nyingi zaidi!

- 66. TINGO** Hii ni rubuni. Tuseme ni asilimia 47 ya jumla ya malipo. Ama ni asilimia 45. Nakuona kuwa mtu mkakamavu wa kushirikiana naye kufanya biashara! Sawa tuseme ni asilimia 40. Hicho ndicho kiwango changu cha mwisho. Upokee au ukatae!
- 67. BEN** Nakushukuru sana kwa kutufikiria sisi na kwa nia yako kutaka kutusaidia kifedha. Lakini hatutaki kufanya shughuli aina hii.
- 68. TINGO** Kama mngekuwa na fedha mngeyafanya yote mtakayo. Lakini utakubaliana nami kwamba hamna jinsi nyingine ya kutenda katika hali mliyo nayo.
- 69. BEN** Hapo umenoa! Mimi na marafiki zangu tumeshaamua jambo la kufanya. Na wanakijiji wameunga mkono uamuzi wetu.
- 70. TINGO** Haya! Sawa! Sitang'ang'ana nawe ila tu nakwambia pendekezo langu hili lipo na litakuwepo kiasi mwezi mmoja hivi ujao.
- 71. SFX: A CHAIR BEING MOVED – STEPS WALKING AWAY**
- 72. TINGO** Usiondoke hivyo! Tayari nimeagiza chakula chetu wawili. Hatuko kijijini! Chakula hapa safi na kimepikwa kikapikika!
- 73. BEN** **(going away)** Asante. Mimi sihisi njaa! Kila la heri!

----- MUSIC -----

Scene 3: In the countryside. Afternoon.**BEN AND NANA.**

74. ATMO: IN THE COUNTRYSIDE. AFTERNOON. BIRDS, CRICKETS

75. SFX: STEPS (TWO PEOPLE) ON THE DRY GRASS

76. BEN Hapa tunaona jinsi mkondo wa maji unavyodhuru udongo. Tunahitaji madimbwi madogo madogo ya maji ili kuzuia mmomonyoko wa udongo na pia kuhifadhi maji. Lau tungekuwa na maji kila wakati, tunaweza kufanya makubwa hapa.

77. NANA Lakini hatuna uwezo wa kuitekeleza kazi yote hiyo.

78. BEN Hilo ni kweli... sasa hivi hatuna namna... Lakini ninaamini tunaweza kufanya mambo mengi. Tunahitaji kuwa wakakamavu...

79. NANA **(LAUGHTER)**

80. BEN Nini kinachokuchekesha?

81. NANA Unaposema tuwe "wakakamavu".

82. BEN Alaa! Mbona?

83. NANA Tumekuwa tukitembea kwa muda wa saa moja. Najua una jambo jingine unalotaka kuniambia...

84. BEN Eee...Ni... ndiyo... kweli... Nilitaka tupate nafasi ya kuwa wawili peke yetu. Peke yetu.

85. NANA Mimi pia. Kwani unaogopa tusionekane pamoja?

- 86. BEN** Wajua jamii ilivyo. Binadamu walivyo. Wanakusingizia mambo yasiyo na msingi. Na hilo linaweza kutia dosari sifa zetu pamoja na chama chetu cha ushirika.
- 87. NANA** Usemayo ni kweli lakini pia si vizuri kujificha. Wala haiwezekani kuweka siri. Ninakuhakikishia kuwa watu zaidi ya 10 tayari wametuona kwa mbali. Sasa hivi si ajabu wameshaanza kusambaza umbea kijijini. Kazi bure kujificha kichakani. La muhimu kuwatanabahisha watu wetu kwamba uhusiano wetu ni wa dhati na madhubuti. Ikiwa tuna uhusiano kweli...
- 88. BEN** Kwani una shaka?
- 89. NANA** Mbona huthibitishi basi?
- 90. BEN** Subiri!
- 91. SFX: RAPID STEPS ON THE DRY GRASS**
- 92. BEN** ...Unaona. Wewe ndiye unayeogopa!
- 93. NANA** Ndiyo! Usiku umeshaanza kuingia. Twende zetu.
- 94. SFX: STEPS ON THE DRY GRASS**

Outro:

Na huo ndio mwisho wa *Learning by Ear* hii leo. Hicho ni kipindi cha sita cha “Kukabiliana na Wimbi la Mabadiliko”, mfululizo wa vipindi kuhusu uhamiaji mijini. Tunakushukuru kwa kutusikiliza.

Wahusika wetu wanaendeleza harakati zao kijijini. Wanakabiliwa na matatizo ya kifedha. Vipi kuhusu mapenzi kati ya Ben na Nana? Je kundi hilo litafanikiwa kuondoa vizingiti vinavyoelekea kutatiza chama chao cha ushirika? Kwa mengi zaidi, usikose kusikiliza kipindi kijacho.

Ikiwa unataka kukisikiliza tena kipindi hiki au kutupatia maoni yoyote fungua ukurasa wetu wa tovuti dw-world.de/LBE au utuandikie barua-pepe kupitia anwani yetu lbe@dw-world.de.

Usisahau kukitegea sikio kipindi kifuatacho!

END OF EPISODE 6